# MKATABA WA MAUZIANO YA SHAMBA

MKATABA HUU umefanyika leo tarehe 28 Mwezi April, 2023 hapa NJOMBE

**KATI YA**

**BENARD DAUDI MWANGALAWE** Mkazi wa Mbalizi Mtaa wa Mtakuja Mbeya wa S. L. P 818 Mbeya, Simu Na…………………(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "MUUZAJI") neno ambalo hakuna budi litajumuisha warithi wake na watu wote wanaoweza kurithi kwa jina lake kwa upande mmoja,

**NA**

**RAPHRAJ ENTERPRISES LTD wa** S. L. P 60386 Dar es Salaam. (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "MNUNUZI") neno ambalo hakuna budi litajumuisha warithi wake na watu wote wanaoweza kurithi kwa jina lake kwa upande mwingine.

**<u>KWA KUWA:</u>**

(a) MUUZAJI ni mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa hekari mia moja (100) lililoko katika Kitongoji cha Kuiji Mgala, Kata Ihanga- Luwenga , Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Njombe.

(b) MUUZAJI ana nia ya kuuza Shamba hilo kwa Mnunuzi katika mkataba huu kwa thamani ya shilingi milioni sitini tu (Tshs 60,000,000/-) na MNUNUZI yuko tayari kununua hilo shamba kwa kiasi hicho cha fedha kinachotajwa hapo juu.

(c) MUUZAJI yuko tayari kupokea kiasi cha Tshs30,000,000/-) ambayo ni sehemu ya fedha ya manunuzi ya shamba hilo kutoka kwa mnunuzi wakati wa kusaini mkataba huu kama malipo ya awali

(d) MNUNUZI yuko tayari kulipa milioni 15,000,000/- leo tarehe 28/04/2023 wakati wa kusaini mkataba huu na shillingi 15,000,000/ nyingine zitalipwa mnamo au kabla ya tarehe 02/05/2023

(e) Bakaa ya milioni 30,000,000/-italipwa baada ya uhakiki wa mipaka na uhalali wa umiliki wa shamba toka kwa Muuzaji na majirani waliomuuzia Muuzaji hapo awali na uthibitisho wa uongozi wa kijiji kuhusu umiliki

BASI MKATABA Huu unashuhudia yafuatayo:-

1. MUUZAJI ameuza na MNUNUZI amenunua shamba tajwa kwenye mkataba huu lililoko kitongoji cha KUIJI MGALA, kata ya Ihanga –Luwenga, wilaya ya Njombe – Mkoa wa Njombe kwa kiasi cha shilingi milioni sitini(60,000,6000/, lakini kiasi ambacho Muuzaji anakiri kukipokea leo ni tsh 15,000,000/- kwa kuweka saini yake kwenye mkataba huu
2. Malipohaya na yaliyobaki yatalipwa kama ilivyokubalika na yatapitia kwenye akaunti ya benki ya Muuzaji ambayo atampatia Mnunuzi

3. KWAMBA shamba lililouzwa lina mipaka ifuatayo:-
    i) Kaskazini – Mto Mdoda
    ii) Kusini – Mtalikidonga
    iii) Mashariki – Barabara na shamba la familiya IWIWA
    iv) Magharibi –Mto Kihewe/Benet Mdamu

4. KWAMBA mauziano haya yataridhiwa na mke wa Muuzaji kwa kuweka saini na picha yake kwenye Mkataba wa mauziani baada ya taratibu zote kuwa zimekamilika kama ilivyoelezwa kwenye mkaataba huu.

KWA USHUHUDA WA HAYA, wahusika wametiliana saini zao kama inavyoonekana hapa chini

**UMETIWA SAINI** na **KUTOLEWA KWANGU** hapa Njombe na **BENARD DAUDI MWANGALAWE**
Ambaye ametambulishwa kwangu na
.............................................................
Ambaye namfahamu leo
Tarehe ...28....mwezi April , 2023

............................................
MUUZAJI

**SHAHIDI WA MUUZAJI**
Jina ISHAKA Lameck..............
Sahihi ....................................
Anuani ......0742 764694...........
Wadhifa ...Mdogo wake...............

**MBELE YANGU**
Jina ...George Kato Mushumba
Saini ........................................
Anuani ..SLP 10855 DSM
Cheo ........WAKILI.........

GEORGE K. MUSHUMBA
ADVOCATE
NOTARY PUBLIC
&
COMMISSIONER FOR OATHS
P.O.Box 10855, DAR-ES-SALAAM

**UMETIWA SAINI**na LAKIRI ya**RAPHARAJ ENTERPRISES LTD** hapa Njombe
Tarehe ...28....Mwezi April, 2023

..................................
LAKIRI

Jina .....................................................................
.....................................................................Sahihi
Anuani ..................................................
Wadhifa ....................................................
...........................................................

# FARM NO .... AT MGALA VILLAGE NJOMBE TOWN COUNCIL

